

Kauli ya Mhariri

Journal of Kiswahili Studies (JSS) ni jarida la kwanza na la kipekee la Kiswahili kwani ni zao la Muungano wa Chuo Kikuu cha Pwani na TUSIMA, (RISSEA). Muungano huu unanua kuendeleza utafiti wa masuala ya lugha ya Kiswahili, ikiwemo Asili, Historia na maendeleo ya Kiswahili, Utamaduni wa Waswahili, Fasihi na Isimu ya Kiswahili.

Makala yaliyochapishwa katika jarida hili yametoka sehemu mbalimbali za ulimwengu na yamechunguzwa na kutathminiwa na wasomi katika nyanja mahsusi. Jopo la wahariri lilishughulikia makala haya kwa dhati na kuhakikisha kwamba masharti ya watathmini yamefuatwa.

Jambo la kuzingatia ni kwamba huu ni mwanzo tu na mengine ya usomi na utafiti yako njiani. Jarida hili ni chombo chetu cha usomi na kila mchango uliofanywa na utakaofanywa utaweza kuleta ufanisi katika lugha ya Kiswahili. Ni matumaini yangu kwamba jarida hili litaweka msingi mkuu wa tafiti za lugha ya Kiswahili na kuiendeleza na kuieneza lugha hii hadi kwenye upeo ya dunia.

Prof. Rocha Chimerah

Chuo Kikuu cha Pwani,

MHARIRI MKUU

